# MWITO WA IKISIRI

## KONGAMANO LA KIMATAIFA LA 11 LA CHAUKIDU

### CHUO KIKUU CHA MAKERERE – KAMPALA, UGANDA

CHAUKIDU

Chama cha Ukuzaji wa Kiswahili Duniani

MAKERERE UNIVERSITY

*We Build for the Future*



**10-13 DESEMBA 2026**




**Mada Kuu:**

**Kiswahili na Lugha Nyingine Afrika: Mustakabali wa Ndani na Nje ya Mipaka ya Darasa katika Dunia Inayobadilika**

Dunia inabadilika kwa kasi kubwa. Utandawazi, mapinduzi ya kidijitali, na mabadiliko ya kijamii na kiuchumi vinaendelea kuziathiri lugha zote. Kiswahili, pamoja na lugha nyingine zisemwazo na kufundishwa barani Afrika na kwingineko, zinaguswa moja kwa moja na mabadiliko hayo, huku umadhubuti wa sera, utoshelevu wa rasilimali, na uhai wa lugha nyingi vikiendelea kutikiswa. CHAUKIDU inawaalika watafiti, walimu, wataalamu wa teknolojia, watunga sera, wadau mbalimbali, na wasemaji wote wanaojali mustakabali wa lugha katika zama hizi kushiriki katika mjadala utakaofanyika katika **Kongamano la 11 la Kimataifa la Kiswahili.** Tunalenga kubadilishana maarifa, kujadili matokeo ya tafiti, na kupanga mikakati ya kuimarisha matumizi, ufundishaji, na maendeleo ya lugha hizi katika zama hizi za mabadiliko.

**Kamati ya maandalizi** inakaribisha ikisiri zinazoangazia maeneo mbalimbali yakiwemo: ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili na lugha za Kiafrika; teknolojia na Akili Ige (AI); lugha za Kiafrika katika elimu ya awali, sekondari, na ya juu; matumizi ya lugha nje ya darasa; lugha za Kiafrika katika vyombo vya habari, biashara, na diplomasia; tafsiri, ukalimani, na maendeleo ya istilahi; sera za lugha na upangaji lugha; uhifadhi na uendelezaji wa lugha zilizo hatarini; fasihi, utamaduni, na utambulisho katika ulimwengu wa kisasa; lugha za Kiafrika katika diaspora na mawasiliano ya kimataifa; na ujasiriamali wa lugha na uchumi wa lugha.

Unakaribishwa kuwasilisha **ikisiri** ya **maneno 200 - 250**, ukibainisha wazi mada, lengo kuu, mbinu, na mchango unaotarajiwa. **Ikisiri** zote ziandikwe kwa kuzingatia mojawapo ya mada ndogo zilizoorodheshwa hapo chini, huku zikiwianishwa na mada kuu ya kongamano.

1. Nafasi ya Kiswahili na Lugha Nyingine Afrika na Kwingineko katika Ushindani wa Kimataifa.
2. Matumizi ya Kiswahili katika Jamii: Nyumbani, Kazini, Biashara na Huduma za Kijamii.
3. Vyombo vya Habari, Mitandao ya Kijamii, na Maudhui ya Kidijitali katika Kupanua Matumizi ya Kiswahili.
4. Vijana, Ubunifu, na Mabadiliko ya Kiswahili.
5. Kiswahili na Lugha nyingine: Ushirikiano, Ushindani, na Mustakabali wake.
6. Nafasi ya Kiswahili katika Sera na Utawala wa Lugha Barani Afrika na Kimataifa: Mchango na haja ya kuwa na Asasi za Kiswahili.
7. Kiswahili kama Nyenzo ya Uchumi na Ujasiriamali.
8. Ufundishaji wa Kiswahili Ndani na Nje ya Mfumo Rasmi wa Elimu: Fursa na Changamoto.
9. Kiswahili na Diaspora: Utambulisho, Uhamiaji, na Urithi wa Lugha.
10. Kiswahili katika Sanaa, Tafsiri, na Ukalimani: Fasihi, Muziki, Filamu, na Mawasiliano ya Lugha.



**KUTUMA IKISIRI**
www.makongamano.chaukidu.org

**MAKATAA**
Julai 18 2026

**KWA MASWALI**
secretariat@chaukidu.org